# HALMASHAURI YA WILAYA KISARAWE
# SHULE YA SEKONDARI JOKETI MWEGELO

**Mkuu wa Shule: 0755 945 229**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0758 187 011**

**Matron: 0756 624 285/0788 298 072**

**Shule ya Sekondari JOKATE MWEGELO**

**S.L.P 28001**

**KISARAWE - PWANI**

**Tarehe :14/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JOKATE MWEGELO HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE MKOA WA PWANI MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………… 
Shule ya Sekondari JOKATE MWEGELO ipo umbali wa Kilometa 65 Kusini mwa jiji la Dar es salaam panda daladala zinazoelekea **kigogo sokoni (stendi ya msanga)** kasha panda gari zinazoelekea msanga/maneromango na shukia kituo cha changombe getini, kasha panda pikipiki itakayo kuleta hadi shuleni Jokate mwegelo sekondari, usafiri wa basi toka kigogo sokoni hadi changombe getini ni shilingi elfu tano (5000) , pikipiki toka changombe getini hadi shuleni ni shilingi elfu tatu(3000) tu.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 vazi rangi DARK BLUE MESS rinda boksi ya V iwe ndefu yenye kuvuka magoti mchoro wa mshono umeambatanishwa mwishoni mwa fomu hii.
ii. Mashati 2 meupe ya shule yenye mikono mirefu na mfuko upande wa kushoto
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni NYEUPE ya kuvaa darasani na KIJIVU ya kuvaa nje ya muda wa darasani ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni track suti angalau jozi 2 rangi DARK BLUE yenye mstari mweupe pembeni na nguo za mchezo wa netball angalau jozi moja rangi dark blue
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
vii. Sweta la rangi ya grey
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) 2 mshono wa marinda boksi rangi ya MAROON iwe ndefu yenye kuvuka magoti na isiyobana
ix. Tai ndefu
x. Tisheti (T-shirt) zenye nembo ya shule vazi la nnje ya darasani angalau 2 yenye shingo ya mviringo 1 na yenye kola vazi la siku maalum 1
xi. Koti la suti rangi ya DARK BLUE MESS liwe na kifungo kimoja mbele
xii. Laboratory coat nyeupe

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari quire 4 zisipungue 12
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika orodha imeambatanishwa mwishoni mwa fomu hii
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro futi $(2^1/2)$.
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1 rangi ya pink, chandarua 1 cha pembe 4 rangi nyeupe
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe ziwe za mfupa zisiwe za mpira, kijiko na chupa ya kuhifadhia maji ya kunywa
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na kubwa moja (lita 20) yenye mfuniko
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani, mfagio 1 wa nje wenye mpini mrefu, panga 1, mfagio mgumu mkubwa na mdogo wa kusafishia

sakafu ya chooni, na sqeezer kwaajili ya kusukumia maji wakati wa usafi.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango ilipwe Benki ya NMB tawi la kisarawe au tawi lolote la NMB nchini kwa akaunti namba <u>21410019639 jina la akaunti ni: JOKETI MWEGELO SEC SCHOOL.</u>**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kuvaa mavazi tofauti na sare zilizo elekezwa, vile vile haruhusiwi kutumia manukato ya aina yeyote.**

- ❖ **Kuepuka kukosea sare fanya mawasiliano kwa namba zilizopo kwenye fomu hii.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Picha (passport) za mwanafunzi atapiga shuleni.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

# HALMASHAURI YA *WILAYA YA KISARAWE PWANI*

***SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JOKATE MWEGELO FOMU YA KUKUBALI SHULE***

### *A. SEHEMU YA MWANAFUNZI*

*1. Mimi (Majina kamili) ……………………………………………………………..*
*Nimekubali kuingia kidato cha ................ katika Shule ya Sekondari ya wasichana Jokate Mwegelo Kuanzia tarehe ……………… hadi nitakapomaliza kidato cha ……………*

*2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.*

*3. Tarehe ya kuzaliwa………………………..Kijiji…………………………………..*
*Tarafa…………………………………….. Wilaya ……………………………Mkoa…....................*
*Shule unakotoka …………………………………..Namba yako ya mtihani………………………..…*

*4. Kituo cha gari (Bus) au Gari la Moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako………………..*

*5. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ..................... Sahihi ya mwanafunzi……………….*

### *B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI*

*1. Mimi (majina kamili) …………………………………………………… simu ..............................*
*ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Jokate mwegelo kuanzia kidato cha ………………………hadi atakapomaliza kidato cha ……………*

*2. Jina kamili la Mama ……………………………………………simu………………………………..*
*Kazi ya Baba ………………………………………..*

*3. Kazi ya Mama ………………………………………*

*4. Anwani ya Mzazi/Mlezi ………………………………*
*………………………………………………………*

*5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaweza kumsaidia wakati wa dharura*

| *Jina kamili* | *Mahusiano* | *Anakoishi* | *Simu yake* |
|---|---|---|---|

*(i)…………………….... …………….. …… ……………………. …………… ………………………..*

*(ii)…………………… ……………..………. ……………………. ……………………………………*

*(iii)……………………. …………………….. ………………….. …………… ……………………….. ..*

*(iv)………………………………………………………………………………………………….*

*6. dhehebu la Dini ya Mtoto ni*
*Lutheran/Katoliki/Anglican/PAG/TAG/ Moravian /SDA/Mwislam*

*7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa :……………………………………*
*Sahihi ya Mzazi/Mlez……………………………….. Tarehe ………………………………..*

**STUDENTS MEDICAL EXAMINATION FORM**

*To be completed by a Medical Officer*

*…………………………………………. (Insert name of* ***the*** *Government Medical Institution) Name of Student ………………………………………………. Form …………… Year ..............*

*Age…………………Sex ............................................. Blood count …………………………….*

*Stool ……………………………………….. Urine ……………………………… …………..*

*T. B. Test ……………………………………. Eyes………………………………………………………*

*Ears ......................................................................................................Chest …………………………………...*

*Spleen ………………………………………………………Abdomen .......................................................*

*Teeth ……………………………………………………………………………*

*Additional information:- (*e.g.pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic family diseases).

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

***I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School.***

*Name of Medical Officer ………………………………….Signature........................Designation.............................*

*Station & Official Stamp…………………………………..       Date …………………………..*

Sharti mtoto apimwe kikamilifu kabla ya daktari kujaza fomu hii. Ikigundulika kuwa daktari alijaza fomu hii bila vipimo kufanyika, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria na za ukiukaji wa haki za binadamu.

***MZAZI/MLEZI mwenye uwezo mnunulie mwanao vitabu kulingana na masomo anayochukua. Orodha ya vitabu ni kama inavo onekana hapa chini***

| ***IDARA*** | ***JINA LA KITABU*** | ***MWANDISHI*** |
|---|---|---|
| ***GENERAL STUDY*** | • GENERAL STUDIES FOR A LEVEL | ***TIE (TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION)*** |
| ***CHEMISTRY*** | • PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL<br>• GENERAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL<br>• IN ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL<br>• ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL<br>• CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL | ***TIE (TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION)*** |
| ***PHYSICS*** | • PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL FORM SIX<br>• PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL FORM 5 | ***TIE (TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION)*** |
| ***BIOLOGY*** | • BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL STUDENTS BOOK FOR 5<br>• BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL STUDENTS BOOK FORM 6 | ***TIE (TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION)*** |
| ***BAM*** | • BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR FORM 5<br>• BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR FORM 6 | ***TIE (TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION)*** |
| ***GEOGRAPHY*** | • PRACTICAL GEOGRAPHY<br>• PHYSICAL GEOGRAPHY<br>• PRINCIPLES OF PHYSICAL GEOGRAPHY | ***TIE (TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION)*** |

*SHAMBA DRESS MUONEKANO WA MBELE NA NYUMA (**RANGI YA MAROON)***



***MSHONO WA SIKETI NA KOTI, KITAMBAA DARK BLUE MESS***






**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA
JOKATE MWEGELO
KISARAWE

**MARIAM K. MPUNGA**
**MKUU WA SHULE**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0755 945 229**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0758 187 011**
- **Mwandamizi Taaluma : 0762 957 011**
- **Mwandamizi Malezi: 0765 769 736/0765 339 965**